CAB. 263/312/07 TIC Report.

(1) DG-TIC

Nipatie taarifa kamili juu ya jambo hili.

Waziri

WUUVB

29/04/2022

KANDEKE FOUNDATION

S.L.P 1271

KIGOMA

17/04/22

(2) NKM-U

Fuatilia na nipate mrejesho kwa haraka

Waziri

WUUVB

29/04/

MKURUGENZI MTENDAJI

KITUO CHA UWEKEZAJI

TANZANIA (TIC)

S.L.P 938

DAR-ES-SALAAM

**YAH: KUNYIMWA HAKI YA KUENDELEZA ENEO LA SHAMBA LUGUFU WILAYA YA UVINZA KIGOMA**

Kichwa cha habari hapo juu chahusika,

Mnamo tarehe 17/07/2017 **Kumb.TICC/B.10/17/132** na 17/04/2020 nilipokea barua yenye **Kumb.Na.TIC/B.10/17/KIG/68** ambayo ilinieleza kuwa Mkurugenzi mtendaji hakuridia maombi yangu ya kumilikishwa ardhi iliopo lugufu wilaya ya uvinza-Kigoma.

Maombi yangu yalikataliwa kwasababu eneo limetengwa kwa ajili ya uwekezaji mkubwa wa kilimo cha michikichi na sio uwekezaji mdogo.Lakini kwenye barua yangu ya maombi nilieleza kua nitafanya uwekezaji wa michikichi (large scale) kama ilivyo kusudiwa. Chakusikitisha barua yangu yakukataliwa ombi langu inasema niliadhimia uwekezaji mdogo kwenye kilimo cha ufuta.

2. MU

Fuatilia kwa ipasavyo tupate mrejesho haraka

NKM-U

02/5/2022

Kampuni yangu **Kandeke Foundation** now ( Sky Mwamoto Ltd) haijasajiliwa na kituo cha uwekezaji **(TIC)** k na kuhusu kusajiliwa ningeomba kupewa utaratibu wakujisajili ili niweze kuendelea na uwekezaji.

Pia ningeomba nikumbushe wizara ya uwekezaji pamoja na kituo cha uwekezaji **(TIC)** kua mnamo tarehe 21/09/2017 nilipewa barua kutoka ofisi ya tawala za mikoa na serekali za mitaa**(TAMISEMI)** yenye **Kumb.Na GB199/203/01/29** ilio elekeza kua Kandeke Foundation inaruhusiwa kuendeleza shamba hilo.Kwa uthibitisho zaidi naambatanisha barua hizo.Kwamasikitiko makubwa niliambiwa niondoke na kwamba sipo kihalali na tayali zaidi ya million miambili (200,000,000 tshs) zimewekezwa pale kwa kuandaa shamba na vifaa kwa ajili ya kuendeleza shamba hilo.

Kwa kumalizia nigeomba wizara husika pamoja na uongozi wa kituo cha uwekezaji(TIC) wanimilikishe eneo hilo ili niweze kuendelea na uwekezaji.

Natanguliza shukrani.

Terry Mwamoto Kandeke

Nakala

**wizara ya uwekezaji viwanda na Biashara**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

# TANZANIA INVESTMENT CENTRE

Telegraphic Address: "INVEST"
Tel: No: (255)-22-2116328
Fax: (255-22) -2118253
E-mail: information@tic.co.tz
Website: www.tic.co.tz
In reply please quote:
Ref. No: TICC/B.10/17/132

Shaaban Robert Street
P.O. Box 938,
DAR ES SALAAM.

24/07/2017

Country Director,
Kandeke Foundation,
P.O. BOX 1271
**KIGOMA.**

**RE: APPLICATION FOR LAND OWNERSHIP IN LUGUFU, UVINZA DISTRICT IN KIGOMA**

Reference is made to your letter dated 17/07/2017 with the above subject, in which you are requesting to be granted ownership of the said land, and you have further revealed your engagement in developing the land for the last four years.

I would like to inform you that it is against the law to start working in the Land which does not belong to you or without official/legal documentation.

However, TIC has started a process of terminating the lease agreement between the Centre and Agrisol Energy Tanzania Limited. Once the process is over, the land will be given to an investor that qualifies for TIC Certificate of Incentives, after the whole process of project evaluation is done and Certificate is issued.

Please be informed accordingly.

**TANZANIA INVESTMENT CENTRE**

Geoffrey I. Mwambe
**EXECUTIVE DIRECTOR**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA
Simu Na: (026) 2322848, 2321607,
2322853, 2322420,
Nukushi: (026) 2322116, 2322146.
2321013,
Barua pepe:ps@tamisemi.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:-

*Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa*
*na Serikali za Mitaa,*
*Jengo la Mkapa,*
*S.L.P 1923,*
*2 Barabara ya Hospitali,*
*41185 DODOMA.*

Kumb. Na: GB.199/203/01/29

21 Septemba, 2017

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza,
S.L.P 12
**KIGOMA.**

Yah: **MALALAMIKO YA KUFUKUZWA KWENYE SHAMBA LILILOPO ENEO LA LUGUFU UVINZA**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

Nimepokea barua ya malalamiko (isiyokuwa na Kumb. Na. wala tarehe) kutoka *KANDEKE FOUNDATION* ikilalamikia hatua ya Halmashauri ya Uvinza kuwafukuza katika shamba lililopo eneo la Lugufu – Uvinza kwa uonevu (*Kiambatisho*).

Aidha, baada ya kuisoma barua hiyo ya malalamiko na kuongea na wewe Mkurugenzi, nimegundua kuwa halmashauri haikutenda haki katika hatua yake hiyo ya kuwafukuza *Kandeke Foundation* kwa sababu zifuatazo:-

1) Eneo linalolalamikiwa linamilikiwa na NGO ambayo tangu imilikishwe haijaendeleza shamba hilo. Aidha, halmashauri ina mpango wa kuwanyang'anya wenye NGO hiyo ili kuwapa wawekezaji wengine.
2) Kuna baadhi ya wawekezaji bado wapo wanafanya uwekezaji wa kilimo katika eneo hilo lakini hawajafukuzwa.
3) Halmashauri ndiyo iliyowapa *Kandeke foundation* eneo hilo la shamba.

Kwa kuwa eneo hilo linamilikiwa kihalali na NGO, wote waliopo eneo hilo walistahili wasiruhusiwe kulima katika eneo hilo. Hata hivyo kwa kuwa wenye shamba hilo wamelitelekeza, mpango wa halmashauri ni kuwanyang'anya, waacheni wawekezaji waliopo waendelee kulima lakini wasijenge majengo ya kudumu wala kupanda mazao ya muda mrefu kama kahawa, miti n.k.

Nitapenda kupata taarifa ya jinsi suala hili lilivyomalizwa na halmashauri bila kuleta mgogoro. Nipate taarifa hiyo kabla ya **tarehe 5 Oktoba, 2017**.

Eng. Mussa I. Iyombe
**KATIBU MKU**

Nakal